



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

**MKOA WA KILIMANJARO**

Simu : 27-29 74369  
Fax : 27- 29 74368  
Email: [ded@haidc.go.tz](mailto:ded@haidc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya Hai,  
3BR-TTCL-Kanisani,  
25382. Bomang'ombe,  
S.L.P. 27,  
**HAI KILIMANJARO**

Kumb.Na.LG/S.10/1/153

Tarehe: 31/07/2024

**TANGAZO LA KAZI YA MKATABA WA KUJITOLEA**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Hai anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Hospitali ya Wilaya ya Hai kuomba nafasi (03) za kujitolea kwa mkataba kwa kada mbalimbali kama ilivyo ainishwa hapa chini.

**1.0 DAKTARI DARAJA II (NAFASI 02)**

**1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Wawe wenye Shahada ya Udaktari kutoka Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza mafunzo kazi "**Internship**" ya muda usiopungua miezi kumi na miwili na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

**1.2 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura
- ii. Kutoa na kusimamia elimu ya afya pamoja na kuboresha afya ya jamii
- iii. Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa  
Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekeza katika misingi ya MTUHA
- iv. Kupanga na kutathimini huduma za afya katika eneo la kazi
- v. Kufundisha wanafunzi na watumishi waliopo kwenye eneo la kazi

- vi. Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi walio chini yake
- vii. Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo
- viii. Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake
- ix. Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement)
- x. Kutoa huduma za outreach katika Wilaya
- xi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

## **2.0 MSAIDIZI WA HESABU (ACCOUNTS ASSISTANT) - NAFASI (01)**

### **2.1 SIFA ZA MWOMBAJI:**

Kuajiriwa wenye Cheti cha Astashahada au stashahada ya Uhasibu kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali au Cheti cha ATEC I kinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA. Waombaji wawe na uzoefu wa kazi zaidi ya miaka (02) na kuendelea katika fani hiyo.

### **2.2 KAZI NA MAJUKUMU**

- i. Kuandika na kutunza "register" zinazohusu shughuli za uhasibu;
- ii. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha
- iii. Kutunza majalada yenye kumbukumbu za hesabu
- iv. Kupeleka barua/nyaraka za uhasibu Benki; na
- v. Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha, Hesabu za Benki na Amana

### **MSHAHARA**

Waombaji watakaopata nafasi na kupewa mkataba wa kazi watalipwa mshahara asilimia hamsini (50%) ya mshahara wa Serikali kulingana na kada husika.

### **SIFA/MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI**

1. Awe Raia wa Tanzania
2. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi umri wa miaka 45
3. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali
4. Kila mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa, kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho wa taifa (NIDA)
5. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika

6. Testmonial” “Provisional Results” Statement of result hati ya matokeo ya kidato cha Nne na kidato cha Sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS**)  
**HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**)
8. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **14 Augosti, 2024**
9. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya Hai,  
3BR-TTCL-Kanisani,  
25382. Bomang’ombe,  
S.L.P. 27,  
**HAI – KILIMANJARO**

10. Maombi yatumwe kwa njia ya posta au yawasilishwe moja kwa moja kwenye Masjala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-**



**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
HAI**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HAI**